*République Démocratique du Congo*

**MINISTERE DE L'ENVIRONNEMENT, CONSERVATION DE LA NATURE ET TOURISME**

---

**DIRECTION DES INVENTAIRES ET AMENAGEMENT FORESTIERS (DIAF)**



# Kitabu Cha Usikivu Mwema Wa Mkataba Ya Kupewa Msitu Kwa Muda

*Mwezi wa sita 2010*

# DAFTARI

I. UFUNGUO ....................................................................................................2

II. NARAKA KISHERIA YA MWANZO ..............................................................3

II.1. Katiba ...................................................................................................3

II.2. Sheria Ya Ndani Inayo – Husu Mgao ..........................................................4

II.3. Sheria Mpango 081 Ya Tarehe 2 Julai 1998 Inayo – Husu Mipango Ya Udongo ....................................................................................................4

II.4. Sheria Inayo-Husu Mgao Wa Udongo ..........................................................4

II.5. Sheria Inayo Husu Misitu Ao Pori (Code Forestier de 2002)...........................5

III. MKATABA WA KUPEWA KWA MISITU ......................................................8

III.1. Nafasi Ya Serkali Ndani Ya Mkataba Wa Eneo La Misitu Inayo Pewa ..........8

III.2. Nafasi Ya Mupewaji Misitu Ndani Ya Mkataba .........................................10

III.3. Nafasi Ya Wakaaji Wa Mahali Katika Mkataba Wa Eneo La Pori ..............14

IV. HAKI NA SHARTI ZA SHIRIKA ZINAZO ELEKEWA ..................................21

IV.1. Serikali Mwenyeji Manufaa ...................................................................21

IV.3. Wakaaji Na Shirika La Nafasi ..................................................................25

V. KWA KUMALIZA.........................................................................................27

VI. VITABU VILIVYO TUMIWA.......................................................................27

VI.1. Niaraka halali .......................................................................................27

VI.2. Vitabu Ao Maandiko Mbalimbali.............................................................28

*Hizi buku zili andikua na mwalimu Kalambay Lumpungu, wa Darasa la sheria ya masomo ma kuu ya Kinshasa, kwa shabaa ya ku onesha somo la kwanza kwa vikundi, matumikisho ya udondo na mazao ya pori. Zili oneshwa na ku hakikishwa na kamati ndongo iliyo undua. Chini ya uongozi wa chumba cha hesabu na matengenezo za pori (DIAF) ya chumba cha waziri wa mazingira Akiba na Matembezi.*

# I. UFUNGUO

Kwa ajili ya kuleta mafunzo kwa vikundi vyote vinavyo husika na matumizi ya sheria ya pori ya mwaka 2002 (Code forestier de 2002) na nyaraka yote ya matumizi hii, Waziri anae husika na manzingira, ulinzi wa misitu na matembezi, ana haja ya kuandika kitabu kinacho husu haki na sharti ya matumizi mbalimbali. Uandishi wa kitabu hiki, ni wa lazima saana kufuatana na usikivu mbalimbali wa wasomaji. Pia umbalimbali kati ya sheria ya sasa na sheria ya asili, na maoni ya mwenyi udongo juu ya msingi huo, italeta kukosa masikilizano katika malumbano, na ni msingi wa mizozo. Kwa hiyo, masemi ya wawekezaji mbalimbali wanayo toa tafsiri yao ya nyaraka.

Haya yote yanatoka kufuatana na habari isiyo heshimu katiba na sheria zingine mbalimbali. Katika matumizi ya sheria inayo-husu misitu na vitabu vya matumizi ya sheria hii, Ofisi inayoangalia pori itafanya ujuviano na masikilizano kati ya wakaaji wa asili juu ya misingi mbalimbali, kama:

- Kukatwa kwa mipaka ya eneo ya pori kwa kazi ya mugao wa misitu;
- Mapatano kwa mambo yanayo angalia ushiriki ulio katika buku la mahitaji;
- Kutungwa kwa mipango ya matengenezo juu ya pori inayo pangwa, eneo ya misitu, na zingine...;
- Kutimizwa kwa uchunguzi wa ushirika na uchumi.

Kazi kama hizo zinaomba mbele, wakaaji waelewe mambo haya, ili waweze kuzungumza juu ya misingi wanayo elewa. Kwa hiyo Ofisi inayo-husika na misitu haipashwe kuacha mambo yasiyo kamilika kufanyika; ao habari kamili ikosekane; kuwasukuma wakaaji kwa nguvu ao tafsiri mbaya ya mambo ya lazima ya maisha ya watu. Ni lazima mbele ya yote kutia nukta juu ya haki na sharti ya vikundi vyote vinavyo elekea matumizi ya eneo la msitu. Ni ya muhimu waziri alete habari kamili na yenye kuelekea mambo yote juu ya msingi huu na kinyume chake chote. Akionyesha njia yenye inayo stahili kufwata na kutia vizuizo. Hakikisho hizi sherti ziandikwe katika buku la tafsiri kwa lugha ya taifa na kujulishwa kwa wakaaji wote, mbele ya kuanza kazi ya ujuvi wowote. Habari hizi zitasaidia vile vile kwa vikundi vyote vinavyo elekewa, waelewe mambo yenye kufanyika, wajue haki na sharti ya kila mmoja: ita epusha ugonvi.

Habari hizi itapelekwa kwanza kwa wakaaji wa asili, juu ya kuwaonesha wazi yote yanayo-husu sheria ya pori, pia haki na sharti zao. Itakuwa vile vile lazima kwa wajumbe wa Waziri ndani ya majimbo, viwanda vyote vinavyo tumikisha pori, kwa wajuzi, kwa mashirika isiyo-kuwa ya serikali na kwa wafanya-kazi wote wenye wataulizwa, waalikwe kwa mabishano juu ya haki za asili, haki ya utumizi, na haki ya udongo.

Kusudi buku hii isaidie kama kitabu cha kuonesha mambo yote na kuya-elewesha mkataba wa eneo ya misitu, inaoneshwa kwa namna hiyo: kwanza naraka kisheria ya mwanzo yenye inaleta tatizo inayo na isiyo-onekana kwa kuelewa mkataba, kiisha nafasi ya kila mmoja ya vikundi vinavyo elekea ndani ya mkataba wa eneo ya misitu na kwa mwisho, kibao cha haki na sharti kwa kila kikundi chenye kuelekea ndani ya mkataba wa eneo ya misitu. Kuna neno la mwisho lenye kukamilisha kwa kifupi.

## II. NARAKA KISHERIA YA MWANZO

Naraka kisheria ya mwanzo itatoshwa ndani ya katiba, ya sheria ya ndani inayo-husu mgao wa sheria mpango juu ya matengenezo ya mtaa na buku la sheria ya udongo na misitu.

### II.1. Katiba

Amri ya 9:

«Serkali ina uwezo wakati wowote juu ya: udongo, maji na misitu, anga, mito, viziwa na vilindi pia bahari ya Congo, na vilima vya bara.»

«Namna ya matumizi na ya kupewa kwa muda, kwa yote inayo kuwa ya serkali yenye kutajwa hapo juu ina fasiriwa na sharia.»

Amri ya 30:

«Mtu wote anae patikana juu ya udongo wa taifa ana uwezo wa kutembea huru, kuchagua makao yake, kuondoka na kurudi katika udongo wa taifa kufuatana na mipango ya sheria. Hakuna mkongomani anae weza kufukuzwa katika udongo wa Jamhuri, ao kukazwa kuishi nje ya nchi ao nje ya makao yake».

**II.2. Sheria Ya Ndani Inayo – Husu Mgao**

Amri ya 66:

«Sekta ni mchango wa wakaaji wa asili mbalimbali zilizo huru, zinazo pangwa kufwatana na asili. Inaongozwa na sultani aliye chaguliwa na anaye pewe mamlaka na serkali.»

«Imeongonzwa kufwatana na yote yapatikanayo katika sheria hii. Hata hivyo vikundi vyote vya asili vinavyo patikana katika sekta hii, vinachunga mipango yao ya asili kufuatana na mipaka na sharti inayo patikana katika sheria hii na sheria inayo-husu viongozi wa asili.»

Amri ya 67:

«Chefferi ni umoja wa wakaaji wa asili walio na asili moja, wanao-pangwa kufwatana na asili, wakisimamiwa na kiongozi anaye chaguliwa kidesturi, mwenye kujulikana na kushimikwa na serikali.»

«Imeongozwa kufwatana na mipango inayo patikana katika sheria hii, pia katika asili isiyo kuwa mbalimbali na sheria na mihuri, pia isiyo leta fujo kwa mipango ya maisha na desturi nzuri.»

**II.3. Sheria Mpango 081 Ya Tarehe 2 Julai 1998 Inayo – Husu Mipango Ya Udongo**

Amri ya 161:

«Kufwatana na sheria mipango, itaitwa mji, kundi lote la wakaaji wa asili wanao pangwa, kufwatana na desturi yao na matumizi ya nafasi, ambayo umoja na masikilizano ya ndani imejengwa binafsi kufwatana na undugu na vizazi. Mji huu umejengwa chini ya madaraka na ulinzi wa kiongonzi anaye julikana na kupewa mamlaka na serkali»

**II.4. Sheria Inayo-Husu Mgao Wa Udongo**

Amri ya 53:

«Udongo ni wa serkali tu, hauwezi kunyanganywa ao kupewa mtu fulani bila ruhusa».

Amri ya 387:

«Sehemu ya udongo ambayo wakaaji wa asili wanaishi, zinakuwa tangu mwanzo wa matumizi ya sheria hii sehemu zao wenyewe».

Amri ya 388:

«Sehemu zilizo za wakaaji wa asili ni sehemu za udongo ambamo wanaishi, wanalima, ao wanatumia kwa namna fulani-binafsi ao kwa umoja, kufuatana na asili ao mila na desturi ya matumizi ya asili».

Amri ya 389:

«Haki ya matumizi wanazo zipata juu ya sehemu hizi za udongo zitafafanushwa na sheria mipango ya Raisi».

**II.5. Sheria Inayo Husu Misitu Ao Pori (Code Forestier de 2002)**

Amri ya 1, muhstari 17:

«Kundi la wakaaji wa asili; ni wakaaji wanao ishi chini ya mipango ya asili na wanao-ungana kwa masikilizano ya undugu na vizazi wakijenga umoja wao wa kati».

Amri ya 7:

«Misitu ni ya serkali, matumizi ya pori na watu ao na viwanda katika sheria binafsi ao sheria ya jumla imetumiwa kufwatana na matengenezo na matumizi ya sheria hii».

Amri ya 9:

«Miti inayo patikana ndani ya mji ao mazingira yake ya kandokando ao ndani ya shamba la kundi ao ya kipekee ni ya kundi lile ao ya mwenye shamba».

Amri ya 88:

«Mkataba wa eneo ya misitu unavipande viwili: mkataba kamili unao julisha haki na sharti ya vikundi vyote, na kitabu cha hitaji zote zinazo eleza sharti rasmi ya mwenye kutumia eneo».

Amri ya 89:

«Ndani ya buku ya mahitaji kunapatikana mafungo kwa jumla na ya binafsi».

«Mafungo kwa jumla ni kwa ajili ya masharti, mbinu yanayo husu matumizi ya vifaa vya lazima».

«Mafungo ya binafsi inaangalia zaidi:

- Pesa za kutumia;
- Sharti zinazo-husu kutiwa kwa viwanda vinavyo pewa kwa mtumizi wa eneo;
- Fungo la upekee inayo-husu kutimizwa miundombinu ya ushirika na uchumi kwa mafaa ya wakaaji wa asili, hasa zaidi: majengo, matengenezo ya njia, kuleta upya vyombo vya hospitali na vya masomo, msaada kwa utembezi wa watu na vitu vyao».

Amri ya 92, muhstari 1:

«Mkataba wa eneo ya msitu umetiwa saini kwa upande wa serkali na Waziri».

Amri ya 9 ya katiba, kwa wale walio fanya usomi wa juu, walifikiria kukanusha sheria ya mbele, ijapokuwa sheria hii ilikuwa iki hakikisha kanuni kuu ya sheria ya mataifa mbalimbali: «Uhuru unao dumu wa mataifa juu ya udongo wao».

Katika mafunzo haya, kwa kuleta mwanga kwa mambo yalio kamilishwa na sheria ya mwanzo, ni ya lazima kuleta hadisi ya masemi hayo. Kwa hivyo tunajiruhusu kuwaletea yote yalio andikwa na mtaalam Nicolas De Sadeleer katika kitabu chake «Vade mecum ya sheria inayo angalia mataifa mbalimbali juu ya utafauti wa maisha-Ulaya-Africa»:

«**Kuacha polepole mawazo ya kuchangia ya ulimwengu, manufaa yenyi kuangalia maisha kwa faida ya uhuru wa taifa**. Kufuatana na mapingano yanayo dumu kati ya mataifa ya kaskazini na ya kusini, kwa ajali ya kujiwekea mambo kazaa yanayo-husu umbalimbali wa maisha, kwa upekee (les genes) sawa vile kupitia haki ya mwenyeji. Mawazo ya kuchangia kwa ulimwengu ilileta shida ya kukosa masikilizano katika matayarisho ya mkutano wa RIO. Mawazo haya, yali achwa na waandishi katika buku la masikilizano kwa mambo inayo-tazama utafauti wa maisha, kwa faida ya mahitaji ya umoja». Hivyo-hivyo, neno «uhuru unao dumu» na uliyo kamili wa kila taifa juu ya manufaa maumbile yake, ilijihakikisha katika mkutano wa RIO. Katika maongezo ya kanuni ya pili, inayo sema kwamba: «Nchi zina haki huru wa kutumia manufaa yao kufwatana na siasa ya mazingira na maendeleo». Sheria ya masikilizano inayo husu utafautili wa maisha ina hakikisha kusema «Inchi zina uhuru wa kutumia manufaa yao kufuatana na siasa yao ya kutumia mazingira».

Neno «Uhuru unao dumu», imetumikishwa saana katika masikilizano ya mataifa kama msemo usiyo badili.

Anapotumikisha uhuru unao dumu na kamili juu ya udongo wake, nchi ya Congo ilikamata kwa tarehe 31/Decemba/1991, sheria n°71-008 inayo-tazama mkaguo wa katiba ya 1967. Sheria hii ina, katika Amri ya 1:

«Imeongezwa katika katiba n°14 bis, maneno kama haya: Udongo na chini ya udongo wa Zaire na yote na pia mazao maumbile ni ya serkali. Sheria ina hakikisha namna inavyofaa kwa kupana na kuyapokea, kwa kuirudishwa ao kuyapana tena. Ila, kurudishiwa ao kuyapana tena haiombi malipo fulani kama mwenye kuyapokea hakuyatumikia».

Sehemu hii katika katiba ilizaa kwa ajili ya udongo, chini ya udongo mazao maumbile, majibu yafwatayo:

- **Udongo:**
  - Sheria n°73-021 ya tarehe 20 julai 1973, inayo angalia kwa jumla matumizi ya vitu, ya udongo na ya vifaa visio ondoshwa, pia matumizi ya uchunguzi: «Udongo ni wa serkali, hauwezi kunyanganywa wala kupewa», Amri ya 53.

- **Chini Ya Udongo:**
  - Sheria mpango ya Raisi n°81-013 ya 2 Aprili 1981 juu ya mipango kwa jumla inayo angalia madini na mafuta:

«Kufwatana na mipango ya katiba, chini ya udongo wote wa Zaïre ni, na inadumu kuwa ya taifa na ina: madini, viwanda vya madini, chemchemu za maji safi na mafuta…», Amri ya 1, muhstari wa 1.

- Sheria 007-2002 ya 11 Julai 2002 inayo husu sheria ya madini:

«Makao yenye kutawaliwa na madini, pia makao ya kuchunga mali ya chini ya udongo, na inayo patikana juu ya eneo ya udongo, ao inayofungwa chini ya udongo, ao katika mito zilizo katika taifa, ni ya serkali tu. Haya wezi kunyanganywa wala kupewaa», Amri ya 3, muhstari 1.

- **Maumbile**
  - Sheria n°82-002 ya 28 Mei 1982 inayo kanunisha mawindo:

«Yenye kuitwa "faune" ni nyama zote za misitu ya aina zote: inayo na isiyo na mifupa…Nyama yenye kunyonyesha, ndege, zinazotambaa chini na aina zote za nyama ya misitu.»

«"Faune" ya Zaïre ni ya serkali tu. Iko ndani ya uchumi wa taifa na inapashwa kutumiwa kwa mafaa ya taifa», Amri ya 2.

- Sheria 011-2002 ya 29 Ogusti juu ya sheria ya misitu:

«Misitu ni za serkali.», Amri ya 7, muhstari wa 1.

Kifupi, tunaweza kusema kama Amri ya 9 ya katiba ikiwa kufwatana na maandiko kama vile mawazo ya waandishi (Watunga sheria) haikatae sheria ya mkaguo wa katiba ya 31 Decemba 1971.

## III. MKATABA WA KUPEWA KWA MISITU

Amri ya 88, 89 na 92 ya sheria ya misitu (Code forestier), inaweza kuitwa mkataba wa eneo za pori, mkataba unao changa vikundi tatu, na kwa hiyo, kutokea uchambuzi wa Amri tatu hizo. Kwa kweli, ndani ya mkataba huu, munamo serkali, mwenye kupewa eneo na shirika ya wakaaji mahali.

Ndani ya mkataba huo wa vikundi vitatu, vikundi vyote vina haki na shurtisho, wa moja kwa wengine.

Ni lazima kujua kama ndani ya mkataba huo, serkali ni kikundi chenye haki nyingi kupita vingine vyote. Kwani, yeye kama vile mwenye misitu, anauwezo wa kutia lazimisho za matumizi bila kuuliza vikundi vingine, kufwatana na siasa ya maendeleo.

### III.1. Nafasi Ya Serkali Ndani Ya Mkataba Wa Eneo La Misitu Inayo Pewa

Serkali ni mmiliki wa udongo, chini ya udongo na vilevile mazao maumbile. Kwa hivyo, yeye ni mwenye misitu, Amri ya 7. Anaweza kuitiya kama vile eneo la misitu. Mpango huu unaweza kutimizwa ao kwa njia ya tenda, ao kwa njia ya mapatano kwa mara, Amri ya 83. Utumizi wa Amri hii sherti ifatanishwe na sheria ya Waziri n°88/09 ya 08 Aprili 2008 yenye kuonyesha mwenendo ya kupana eneo la msitu, iwe kwa njia ya tenda (Amri ya 3 mpaka 36), iwe kwa njia ya kuuza kwa mara (Amri ya 37 mpaka 39).

Ofisi inayo husika na misitu, ina kazi ya muhimu wakati wa kutunga kanuni za mkataba wa kupewa kwa misitu, ambamo buku la mahitaji ni sehemu moja tu ya mkataba[1]. Hakika, uhakimu huu ndio una uwezo wa kuleta kanuni na sharti za matumizi zinazopashwa kuandikwa, iwe ndani ya mkataba wa kupewa kwa misitu, iwe ndani ya buku la mahitaji.

Amri ya 88 ya sheria ya misitu yenye ilitajwa hapo juu, imefasiriwa na sheria ya Waziri ya 7 Ogusti 2008, kibambo cha I. Kibambo hiki kinapanga kwa Amri yake ya kwanza, kama mkataba wa kupewa kwa misitu unatafsiri haki na sharti za vikundi, na ina ongezwa buku ya mahitaji, ambayo ni moja wa mkataba wa kupewa kwa misitu. Amri ya kwanza, kibambo cha II, inaendelea kusema eti buku la mahitaji ni msingi mkuu wa kuhakikisha sharti ya binafsi, yenye sherti itimizwe na mwenye kupewa msitu kufwatana na iliyo semwa ndani ya mkataba wa kupewa kwa msitu.

Yana stahili kubambwa kwa mkataba wa kupewa kwa msitu na kufanya umoja na mkataba huo. Buku la mahitaji, ni cheti cha haki ya sheria cha muhimu, chenye kuonyesha kwa mambo kama haya, sharti maalumu ya mapatano ya vikundi katika mkataba wa kupewa kwa misitu. Ni kusema, Serkali mwenye kumiliki misitu na wakaaji wa nafasi. Kuvunjwa kwa mapatano haya, kuta lazimisha serkali ianze kutafuta namna ya kumuondosha aliepewa misitu, ili yarudishwe kubaki msitu wa serkali. Kwa namna hii, serkali itaweza kuhakikisha mamlaka yake kwa kueshimisha mipango ya matumizi ya misitu na matumizi yake[2].

Amri ya 89, sheria ya misitu (Code forestier) kinapanga: «Buku la mahitaji lina mipango ya kawaida ya jumla na mipango binafsi...». Mipango ya kwanza ni juu ya sharti, mbinu yenye kuelekea matumizi ya mazao yanayo hitajika. Ya pili:

1. Mahitaji ya pesa;
2. Sharti ya yote inayo husu kuwekwa kwa viwanda na yanayo hitajika kwa anayepewa misitu;
3. Mpango wa ushirika wenye kufatana na kutimizwa kwa majengo ya ushirika na uchumi kwa faida ya wakaaji wenye nafasi.

[1] Sheria ya Waziri n°28/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/08 ya tarehe 7 Ogusti 2008 inayo onyesha namna ya mkataba wa msitu ilio pewa kwa matumizi ya mazao ya pori na ya buku ya mahitaji yenye kuyaelekea.
[2] Sheria ya Waziri n°102/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/09 ya tarehe 16 Julai 2009 itiayo mipango ya yote inayo hitajika kwa kuhakiki wa misitu.

Ndani ya mipango binafsi, nukta ya 1. na ya 2. inahusu serkali na anayepewa msitu, nucta ya 3. inahusu anayepewa msitu na wakaaji mahali.

Amri ya 40, sheria ya Waziri ya 8 Aprili 2008, inapanga: «Buku moja ya mahitaji yenye kueleze matumizi ya misitu inayo pewa inaandikwa na Uhakimu inayo husika na mambo ya misitu, kiisha ujuvi wa wakaaji wa nafasi…», na Amri ya 13, muhstari wa 2, kibambo cha II, sheria ya Waziri 028, tarehe 7 Ogusti 2008 inasema: «Uhakimu wa jimbo inayo husika na misitu ya nchi ina kesha kwa ujuvi kweli ya wakaaji wanao itajiwa na inasaidia masikilizano na usaini wa mapatano», na Amri ya 10, muhstari wa 6, kibambo cha I, sheria hii, inasema tena: «…Uhakimu inaweza kuhuzuria ndani ya mikutano ujuvi (ao mapatano)».

Yenye kutoka ndani ya Amri hii ni kusema, uhakimu inatumika kwa ajili ya kutambua shirika mbalimbali la wakaaji wa nafasi wenye kustahili kualikwa kwa mapatano, inakesha kwa kuheshimisha sheria na mipango juu ya mambo haya. Pia, inasaidia ndani ya mwenendo wa mapatano, usawa wa haki wa vikundi vinavyo hitajiwa. Kufuatana na nia hiyo, uhakimu ina muhula wa kusaidia vikundi katika mazungumzo na mapatano.

Vifungo vya mapatano za ushirika, ina fanyika kati ya anayepewa msitu na shirika ao mashirika ya wakaaji wa nafasi, wanao husika na mapatano haya. Kwa kupewa samani, mapatano sherti ziwe na saini tatu: ya vikundi viwili vyenyi kuhusika na mkataba ao wajumbe wao, na ya kiongozi mkuu wa kata, yeye kama vile shuuda.

Serkali itatiya saini yake ndani ya mkataba wa kupewa kwa msitu nyuma, kiisha saini kutiwa ndani ya buku la mahitaji, yapatikanamo vifungo vya jumla, vifungo binafsi na kuwekwa pesa benki yapatikanayo ndani ya Jamhuri ya Kidemocratia ya Congo. Mkataba huu unatiwa saini kwa upande wa serkali na Waziri, Amri ya 92, Waziri anaye husika na mambo ya misitu, Amri ya 1, nucta 9, sheria ya misitu.

**III.2. Nafasi Ya Mupewaji Misitu Ndani Ya Mkataba**

Mwenye kupewa misitu ndie wa lazima saana ndani ya mkataba wa kupewa kwa misitu.

Kufuatana na Amri ya 8 ya sheria ya misitu, mwenye kupewa msitu (Code forestier) ni mtu ao shirika, lenye kukubali kufanya mkataba wa kupewa kwa msitu na serkali, kwa kuyatumia kwa kazi kazaa. Kama vile, kazi yenye kuelekea matumizi

ya mazao ya msitu, inayo saidia kwa kuweka akiba ao kwa matembezi na kwa mawindo. Ao kwa kuvumbua yote inayo maisha. Pia kwa matumizi ya yote inayo kuwa na maisha tafauti. Kufwatana na Amri ya 96 ya sheria ya misitu: «Matumizi ya misitu inasikilika, sio kwa kukata tu ao kwa kuvuna mazao ya misitu, bali pia kwa ajili ya matembezi».

Kanuni ni kusema, kupewa kwa eneo ya misitu kunafanyika kwa njia ya tenda, Amri ya 83, muhstari wa 1. Mtu ao shikirika, anaye ao linalo-weza kualikwa ao kupatikana katika kutafutwa kwa utumizi wa msitu, ao kwa kuchagua mambo inayohusu kupewa kwa eneo ya udongo, anachaguliwa muajibikaji mwenye anapata alama nyingi mbinu na ya pesa. Nkwa hiyo, anakuwa muuzishaji. Hivi, ana siku makumi tatu (30) kwa kuleta akiba ya kuonesha kwamba atatimiza vizuri kazi zake. Asipo-fanya hivyo, ndani ya muda ulio kubaliwa, ao unao faa, mkataba utaletwa kwa muajibikaji alie kuwa wa pili kufatana na alama zake, Amri ya 34, muhstari wa 2[3].

«Msitu wa kukingwa unaweza kupewa, kwa njia ya mkataba, kwa muda usio pita miaka 25. Muda huo, unaweza ongezwa mara mbili kufuatana na sharti ipatikanayo ndani ya mkataba», Amri ya 21, muhstari wa 1, sheria ya misitu.

Amri ya 3, kibambo cha 2, sheria ya Waziri ya tarehe 7 Ogusti 2008, kinashurtisha kwa mwenye atapewa msitu kwa siku zijazo, kutayarisha na kuleta kwa uhakimu unao tazama msitu ginsi atatumia msitu kwa miaka ine ya kwanza zijazo, inayo fata saini ya mkataba wa eneo la msitu atakao-pewa.

Toka siku iliyo tiwa saini ya mkataba mpaka siku ya kukubaliwa kwa mpango wa matumizi, mpewaji wa sehemu ya msitu atatumia msitu ulio kubaliwa na uhakimu akiheshimu mpango wa matumizi iliyo pewa na uhakimu, Amri ya 1 na ya 10, muhstari wa 2, sheria ya Waziri n°28 ya 7 Ogusti 2008. Mpango huu wa matumizi ni mchango wa makubaliano ya mpewaji wa msitu kwa siku zijazo, kwa matumizi ya msitu aliyo pewa, kabla ya kukubaliwa kwa mpango wa matengenezo. Makubaliano haya, yanatoka katika hitaji mbinu, ikiwa kwa tenda ao ndani ya mpango wa kuanziliya, ikiwa kwa vyeti vya kale vya kupewa kwa msitu. Kibaruwa cha makusudio ao garama la akiba inayo hakikisha inayo badilishwa na eneo la msitu.

Masikilizano ya ushirika ndani ya mpango wa matumizi, ao wa buku ya mahitaji mnamo patikana sharti la ushirika la yule anae pewa msitu kwa kundi ao vikundi vya wakaaji wa asili. Kwa kweli mpango wa matumizi unaonesha:

---

[3] Sheria ya Waziri ya tarehe 8 Aprili 2008 inayo-onesha namna ya kupana sehemu ya msitu.

1. Mipaka na taswira ya mazao ya miaka ine ya mbele; pia na kutambua faida ya miaka ine ijayo ya vikundi vyote vya asili;
2. Kufanya kalenda na namna ya ujuvi wa wakaaji wa nafasi juu ya yote yapatikanayo, pia ginsi ya matumizi ya mpango wa ushirika na uchumi, vile vile majengo yanayo faa kwa wakaaji muda wa miaka ine (4) ya kwanza;
3. Ufafanuzi wa kazi za makingo ya mazingira na ukingo yote yanayo maisha mbalimbali;
4. Kuwekwa muda wa miaka ine ya kwanza ya matumizi kwa viwanda vilivyo katika mkataba wa masikilizano.

Mpango huo wa matumizi una saidia kwa nafasi ya buku ya mahitaji, na ya mpango wa matengenezo kwa muda. Kwa sababu, utaingizwa katika buku la masikilizano la mwisho, litakalo bambwa kwa mkataba wa kupewa kwa eneo la msitu, amri ya 10, muhstari wa 4.

Amri ya 7 sehemu ya 2, kibambo cha 2, sheria ya Waziri ya tarehe 7 Ogosti 2008, yanasema: «Kwa kukataa ugomvi unao weza tokea juu ya haki ya utumizi pori, mmiliki wa msitu anaomba maelewano na vikundi vya wakaaji mahali ao na wakaaji wa asili majerani, ambao wana hakikisha haki na sharti ya vikundi vyote, pia na namna ya matumizi». Mpango huu una hakikisha Amri ya 44, sheria ya msitu inayo sema hivi: «Kundi zote za wakaaji jerani wa sehemu ya msitu, iliyo pewa, wanaendelea kuwa na haki ya matumizi yao kawaida katika eneo la msitu, kufuatana na yale yanayo patana na matumizi ya msitu: kuondoa ukulima».

Mpewaji sehemu ya msitu, hana ruhusa ya kuomba malipo fulani kwa ajili ya matumizi haya. Juu ya maelewano yanayo husu haki ya kutumia eneo la msitu ulio pewa, mpewaji msitu kwa siku zijazo, anapashwa kufanya mkataba na wakaaji majerani kwa masikilizano yanayo tazama majengo ya ushirika na uchumi, na kazi ya ushirika ya maendeleo kwa faida yao. Amri ya 13, sehemu ya 2, kibambo cha haya kinasema:

«Masikilizano haya yana husu zaidi:

1. Mpango wa ushirika na uchumi pia viwanda;
2. Kujua nafasi ya wa faidizi wa majengo na kazi;
3. Tarehe ya kutimiza majengo na kazi;
4. Bei inayo fikiriwa kwa majengo na kazi. »

Mpewaji wa msitu anaweza kuwa mtu binafsi ao shirika la watu. Kama ni mtu binafsi, anaweza kusikilizana na kutia saini, mapatano pamoja na kundi ao vikundi vya wakaaji mahali. Kama vile anaweza pia kuwapa barua inayo saini yake, ao inayo saini ya serkali, kwa mtu anaye ruhusa ya kumsimamia. Kama ni shirika, itasimamiwa na mtu aliye chaguliwa na kujulikana katika shirika, kwa kutenda kwa jina na kwa niaba ya shirika. Mjumbe anaweza toa barua ya usimamizi wa upekee kwa mtu mwingine anaye mpendelea kwa ajili ya kazi hizo.

Bila mapatano haya, hakuna saini kwa mkataba wa eneo ya msitu. Kwa kweli, kama mkataba wa eneo la msitu unaweza kukusanya vikundi viwili, kwa mwisho wake, vinakuwa, kwa ajili ya masikilizano ya ushirika, mkataba wa vikundi vitatu. Sababu buku ya mahitaji ni sehemu ya mkataba wa eneo la msitu.

Amri ya 17, sehemu ya kwanza, kibambo cha 1, sheria ya Waziri ya tarehe 7 Ogusti 2008 inasema: «Mpewaji wa sehemu la msitu, anakubali kutia majengo ya ushirika na uchumi, na kupana kazi zamaisha yenye mafaa kwa wakaaji wa nafasi na/ao wakaaji wa asili, ka ginsi imehakikishwa ndani la buku la mahitaji…». Matumizi ya Amri ya 89, sehemu ya 2, nucta C ya sheria ya msitu, inakutana na shida. Ndio maana pahali pa kuacha mpewaji wa msitu kutimiza yote ambayo yanakuwa katika makubaliano, ni bora mpewaji msitu atie mfuko wenye utapokea yote itayopewa bei na kulinganishwa na mazao yote ya mwaka. Wa mwanzo mfuko huu ni akiba ya 10% ya bei ya majengo, viwanda vya ushirika na uchumi ya kipindi cha kwanza cha kazi ya miaka mitano.

Amri ya 15, kibambo cha pili kinahusu mwenye sehemu ya msitu uliotoka katika hatua ya mageuzo ya vibaruwa vya zamani, ya wapewaji msitu. Hivi wa towe:

1. Mpango wa ujuvi (masikilizano) na vikundi vya wakaaji wa nafasi na/ao wakaaji wa asili majerani la eneo la msitu;
2. Mpango wa ushirika na uchumi, pia majengo viwanda kwa faida ya wakaaji wa nafasi na/ao wakaaji wa asili majerani wa eneo la msitu;
3. Kibaruwa chote unao husu mkataba, ao kibaruwa kyengine: wenyi kumuunga na wakaaji wa nafasi na/ao wakaaji wa asili jerani ya eneo la msitu;
4. Mpango wa matumizi mazingira ya eneo ya msitu.

Amri ya 23, sehemu ya 2, sheria ya msitu kinasema: «Misitu za kutoa mazao inayo-dumu, haziaingaliwe na haki zote, na ni huru». Kufuatana na mpango huu, waandishi wa sheria ya msitu inayo tafsiri na kutiwa mkazo, wanasema:

«Misitu inayo toa mazao yenyi kudumu, yameondoshwa katika misitu zinazo kingwa (Amri ya 10, kiisha ujuvi kwa jumla, uno husu wakaaji majerani wa msitu na ipatikanamo sehemu zote, kwa shabaa ya kutambua haki zote zinazo ongezwa juu ya msitu zinazo elekewa».

«Mwenendo wa uchunguzi ni wa lazima. Kama kwa mwisho, imeonekana kama pori fulani sherti iuzishwe, pori hii itaomba kubaki huru, ni kusema, wenye haki juu ya pori hii, sherti walipwe kabla ya kuondoshwa haki yao, kama inavyofanyika na serikali wakati imenyanganya yote yalio chini ya uwezo wake kwa mafaa ya wote[4]. Ni kwa mwisho wa Mwenendo huu, ndiyo wakati sheria za mawaziri wanao elekewa kushimikwa mihuri kwa ajili ya misitu zinazo toa mazao yanayo dumu. Hata vile, lazima kujua kwamba haki ya matumizi ya pori hazi-elekewe na mpango uwo wa kuachwa huru sababu inakuwa masumbuko inayo hakikishwa na sheria»[5].

Ivi kwa yote yanatoka kusemwa, mpewaji wa pori ana sharti zinazo hakikishwa ndani ya buku ya mapatano ya ushirika na wakaaji wa nafasi. Kwa namna zingine, mapashwa ya mpewaji ya sehemu ya pori katika sheria hii nyipia ina kamata nafasi kwa kiwango kikubwa katika sharti za asili, kufatana na kanuni kubwa za sheria «kitu kimoja hakiwezi kulipwa mara mbili».

Lakini, wale wanao pewa pori, kwa njia ya kugeuzwa kwa vibaruwa yao, wanapashwa kueshimu sharti za asili, ingawa awaja saini mkataba hakika wa eneo la pori, na buku la mahitaji.

## III.3. Nafasi Ya Wakaaji Wa Mahali Katika Mkataba Wa Eneo La Pori

Neno hili «Shirika la wakaaji wa mahali» ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika sheria ya udongo kwa vipengele vya 387 na 388, bila kutafsiriwa. Kukosa mwangaza huo kulitimizwa kwa sehemu na mfanya sheria (Code forestier) ya pori katika amri ya 1, nucta ya 17 kama hivi: «Shirika la mahali: ni wakaaji wanao ongonzwa na asili yao na wenye kuungana kindugu kufwatana na vikoo au vizazi vyao, vyenyi kujenga umoja wa kati. Wanajulikana kufwatana na maisha yao katika sehemu ya udongo unao julikana».

[4] Katiba, Amri 34, muhstari wa 1, nucta 24: «Pori iliyo kuwa ya mtu binafsi haiwezi kuguswa. Serkali inasaidia mwenyi pori; ao kundi walio pewa, kufwatana na sheria ao asili…Msitu hauwezi kunyanganywa kwa mwenyeji, isipo kuwa kwa faida ya wote na mbele ya yote kutoa malipo yanayo kubaliwa katika kanuni za serikali.»

[5] V. VUNDU DIA MASSAMBA NA G.KALAMBAY LUMPUNGU**:** Sheria ya msitu iliyo fasiriwa kwa p. 21.

Kundi la wakaaji wanafasi ina vutia pia namna ya uongonzi wa kata.

Ona ginsi sheria ya ndani n°08-016 ya 7 Octoba 2008 inayo husu mpango wa uongozi, muundo na mgawanyo wa uhakimu na mapatano na serikali kuu, pia majimbo, ndiyo inatafsiri: Sekta na chefferi.

- «Sekta ni zaidi mchango wa vizazi vya asili mbalimbali, vilivyo huru kati yao vienyi kupangwa chini ya uwezo wa sheria ya asili. Imeongozwa na sultani anae chaguliwa na ku pewa mamlaka na serikali.

  «Imeongozwa kufwatana na mipango ya sheria hii. Hata vile, mchango wa vikoo vya asili vinavyo yajenga, wana chunga namna yao ya kuishi kufwatana na mipaka na sharti zipatikanazo ndani ya sheria hii na sheria inayo angalia viongozi wa asili», amri ya 66[6].

- «Chefferi ni mchango wa vikundi vya asili moja vyenyi mipangilio kufwatana na asili yao na inayo kuwa chini ya uongonzi wa mtu aliye pewa mamlaka na asili, mwenyi kujulikana na kushimikwa na serikali.

  «Uhakimu wake unafwatana na mipango ya sheria hii na ya asili. Uhakimu huu hauwezi kwenda umbali mbali na sheria, ya muongonzi wa jimbo, ao na amani ya watu wote na tabia nzuri», amri ya 67[7].

---

[6] Fafanusha:
- Sheria n°95-005 ya tahere 20 Decemba 1995 juu ya mgao wa utawala wa serikali, amri ya 107.
  «Collectivite secteur ni sehemu ya uhakimu ndogo inayo chunga vikundi vidogo vidogo vya asili mbalimbali na vilivyo huru, vinavyo ongozwa kufwatana na mazoezo, vinavyo wakaaji wadogo kwa ajili ya maendeleo yao na wanao sultani anayejulikana na kupewa mamlaka na serikali».
  « Collectivite secteur ina uhakimu kufwatana na mipango ya sheria hii kwa yote, vikundi vya ufalme wa vizazi vya mazoezo vilivyo ndani yake, wanachunga asili yao kufwatana na mipaka na kanuni zilizo ndani ya sheria hii».
- Sheria makamu 081 ya tahere 2 Julai 1998 inayo angalia mpango wa udongo na uhakimu, amri ya 140.
  « Secteur ni jumla ya vikundi vidogo vidogo vya wakaaji mbalimbali wa asili zilizo huru, inayoongozwa chini ya mazoezo, lakini ambavyo vina wakaaji wadogo kwa ajili ya maendeleo yao mazuri na iliyo chini ya uongozi wa sultani anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali: Imeongozwa kufwatana na mipango ya sheria makamu hii. Kwa yote, vikundi vya falme za vizazi na mazoezo vinavyo patikana ndani yake, vinachunga kila moja namna yao ya maongozi, vikiheshimu mipaka na kanuni zilizo katika sheria hii».

[7] Fafanusha:
- Sheria n°95-005 ya tahere 20 Decemba 1995 inayo angalia mgao wa inchi kwa uongozi, amri ya 106.
  « Chefferie ni sehemu ya uhakimu unao heshimu mgao wa inchi kwa uongozi, inayo kuwa jumla vikundi vya wakaaji wa asili zinazofanana ao moja, inayo ongozwa na mazoezo na iliyo

Yana tokea kwa mafasirio ma wili ya kwamba wakaaji mahali ni kama wakaji wa kiasili, wanao kiongozi, kua hayo sheria ya serikali ya tarehe 7 oktoba 2008 kwa amri ya 85, sultani wa sekta ndiye kiongozi wa sekta, ni msimamizi wa sekta kwenye chumba cha haki na kwa wengine, kwa yenye ku angalia amri ya 86 ya sharia hii moja inasema; sultani wa cheferi ndiye kiongozi wa cheferi na ni msimamizi wa cheferi mbele ya wengine;

Yanayo angalia sultani wa mazoezo, amri ya 207 kipengele cha 1 na 2 cha katiba kina sema: «Wuongozi wa mazoezo unajulikana kufatana na mazoezo ya mahali, kwa yote si umbali na katiba, sheria, usalama ya watu pia na tabia nzuri…».

Kwa kweli, vikundi vya wakaaji wa asili vinajulikana kupitia vijiji vyao, hivyo amri ya 142 cha sheria ya 20 Decemba 1995 na amri ya 161, sheria ya Waziri ya 2 Julai 1998 inapanga: «Inaitwa kijiji, shirika la asili wanao mipangilio kufuatana na mazoezo yao na mafanyizio yao ya mahali na wenye umoja na kuhusiana kati yao, kufuatana na masikilizano ya vikoo na vizazi».

Shirika lote la nafasi ao wakaaji wa asili ni wenyeji udongo fulani. Sehemu hii iliyo ya wakaaji wote, wanachangia udongo na vyote vipatikanvyo katika udongo, kama vile misitu. Shirika na watu wake wana mamlaka juu ya udongo wao pia haki nyingi zinazo angalia udongo kwa namna na uwezo mbalimbali. Wanamemba wa shirika hii wana changia katika milki hii haki za Kufurahi ya haki hizi ni za kipekee, ni kusema mtu wote anaye ishi katika milki ya shirika ana haki kwa upekee ya yote ambayo sehemu hii ya udongo inaweza kumutolea; kama vile: mawindo, uvuvi, mavuno ya mazao maumbile na kadhalika. Ni ya lazima kujulisha kwamba uhuru na uwezo wa kutumikisha haki za kufurahia za kipekee inapenda kusema kwanza kuwa moja wa wanamemba wa kikundi cha wakaaji wenyi sehemu ya udongo.

---

chini ya uongozi wa sultani wa asili anaye chaguliwa kwa mazoezo, anajulikana na kupewa mamlaka na serikali».

«Imeongozwa na uhakimu kufwatana na mazoezo, bila kwa inje ya mipango ya sheria hii na pia mazoezo hii, isiwe umbalimbali na mipango za sheria ya watu wote, amani na tabia nzuri».

- Sheria makamu 081 ya tahere 2 Julai 1998 inayo angalia maongozi ya inchi na uhakimu, amri ya 141.

« Cheferie ni jumla ya vikundi vya wakaaji wa asili zinazo fanana ao moja, wanao ongonzwa kufwatana na mazoezo na ilio chini ya uongozi wa sultani anayewekwa na asili, anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali».

« Imeongozwa na uhakimu, kufwatana na mazoezo, bila kwenda umbalimbali na mipango ya sheria makamu hii, na pia mazoezo hii, yasiwe umbalimbali na mipango ya sheria, na amani na tabia nzuri».

Juu ya milki ya udongo ya shirika ya mahali ao ya asili, wana ruhusiwa kuishi, wanamemba wa shirika, lakini pia watu walio ingizwa katika shirika kwa njia ya unyumba, kwa kukubaliwa katika kizazi ao kwa mbinu zote za mazoezo na pia wageni. Kwa matumizi ya haki ya kufurahia ya watu wote, hakuna tofauti kati ya mwanamemba wa shirika ya mahali, mwanamemba alie ingizwa na mgeni. Lakini tofauti ni kubwa kwa yale yanayo angalia haki binafsi inayo ondoshwa. Kufuatana na maumbile ya haki ya sheria. Kwa kweli ikiwa watu wote wana uwezo wa kutumikisha udongo, kukinga na kustawishi matumizi inayo toka kwa makubaliano mbalimbali toka ukingo mkuu kufikia ukosefu usio weza kukubaliwa.

Amri mbili ya buku ya sheria ya msitu inafafanua hayo yanayo toka kusemwa:

«Miti zipatikanazo katika kijiji Fulani, mazingira yake jirani, katika shamba la watu wote ao la upekee ni la watu wote ao la mwenyeji wa shamba…», amri ya 9, sehemu ya 1.

«Shirika la nafasi inaweza kwa ombi lake, kupewa kwa kutumikisha sehemu ao kwa jumla misitu zinazo kingwa, katika misitu zilizo chini ya uhakimu wao kufuatana na mazoezo», amri ya 22, sehemu ya 2.

Kama shirika la nafasi haikusaini mkataba wa eneo la msitu wana uwezo kinyume kwa makubaliano yao na mtumikishaji wa eneo ya msitu.

Angalia mifano tunayo yapata kutoka sheria ya Waziri namba 028/CAB/MIN/ECN/15/JEB/08 ya 7 Agosti 2008 inayo hakikisha namna ya mkataba wa eneo kwa matumizi ya manufaa ya msitu na ya buku la mahitaji yapatikanamo.

- <u>KIBAMBO CHA I</u>

- Haki za matumizi ya asili ya shirika la nafasi na/ao wakaaji wa asili wa kandokando la eneo kama inavyo semwa katika amri ya 36, 37, na 44 ya sheria juu ya misitu, lazima ziheshimiwe na mpewaji eneo.

  «Imekatazwa kwa mpewaji wa msitu kuleta mzongano kwa ajili ya matumizi ya shirika la nafasi na/ao waakaji wa asili wa kandokando kwa haki ya matumizi ya msitu namna inayo julikana hivyo», amri ya 6.

- «Mpewaji wa msitu anaitika kujenga yote inayo angalia ushirika na uchumi na kuleta kazi za ushirika kwa faida ya shirika la nafasi na/ao kwa wenyeji wa udongo kama ginsi imesemwa katika buku la mahitaji.»

«Muda wa matayarisho ya mpango wa matengenezo, mpewaji eneo ya msitu anajuviana na wakaaji wa nafasi na/ao wenyeji wa msitu majirani, kwa yote inayo husu mpango wa ushirika na uchumi pia miundombinu, itakayo fanywa buku la mahitaji ya mwisho, na kubambwa juu ya mpango wa matengenezo. Buku hii itatumikishwa miaka mitano inayo fuata kukubaliwa kwa mpango wa matengenezo, na kurudishwa upia kisha miaka mitano ijayo.»

«Hata vile, sehemu ya 2 inayo tajwa juu, mpewaji eneo la msitu anaitika kutumikisha wakati wa majuviano na shirika la nafasi na/ao wenyeji msitu wa kandokando; mpango wa ushirika na uchumi pia miundombinu ya ushirika na uchumi na ya kazi zote za ushirika katika kipindi cha mpango wa matengenezo», amri ya 17.

- <u>KIBAMBO CHA 2</u>

- «Mpewaji wa msitu analeta kwa serikali inayo pana eneo, na ana sainisha naye mpango wa matumizi unao patikana amri ya 10 ya mkataba wa eneo la msitu katika kipindi cha matayarisho ya mpango wa matengenezo. Mpango huu wa matumizi unajulishwa katika vibarua kwa viongozi vya nafasi na ina fasiriwa kwa shirika za mahali nafasi na/ao kwa wakaaji wa asili kwa namna zinazo kamilishwa.»

  «Mpewaji msitu anatimiza mpango wa matumikishi wakati wa matayarisho ya mpango wa matengenezo», amri ya 3.

Ya sheria namba 08/09 ya 8 Aprili 2008 yenye kuweka mwenendo wa kupanwa kwa msitu, amri ya 40 inasema: «Buku la mahitaji yenye kuelekea matumizi ya misitu zenye kupanwa ina hakikishwa na uhakimu unao husu misitu kiisha ujuvi wa wakaaji wa nafasi wanao elekewa, na inapelekwa kwa Waziri ili akubali…».

Niaraka zinasema wazi kwamba buku la mahitaji ni moja ya sehemu la mkataba wa eneo la msitu. Kwa hivyo ikiwa mpewaji msitu haeshimu masikilizano walio kubaliana kwa faida ya shirika Fulani, shirika hili inaweza kumpeleka mbele ya sheria kupitia wajumbe wake wa asili.

Kwa yote yanayo angalia mapatano ya vifungo vya shirika katika buku la mahitaji kati la kundi ao vikundi vya wakaaji wa nafasi na yule atakae pewa msitu, ona inayo andikwa katika buku la sheria ya msitu inayo tafsiriwa na kuhakikishwa:

«Kwa faida ya kuingiza vikundi vyote vya wakaaji wa nafasi katika matumizi ya kushirikiana, na kwa kuonesha uongozi unao faa, vikundi hivi vya wakaaji vilipashwa, katika uhuru, kusikilizana na mpewaji wa msitu, kupitia buku la mahitaji. Ili neno linalo angalia kujengwa kwa viwanda vya ushirika na uchumi, litimize faida yao, na kupitia mawazo hayo, kazi ya uchungi ilipashwa kupewa kwa vikundi vya wafanya kazi wa upekee. Kwa hiyo uhakimu wa msitu utakuwa tu na kazi ya kuongeza mpango huu kama inavyo kuwa katika makubaliano kwa mkataba wa eneo la msitu unao pashwa tiwa saini na Waziri…»

«Ingelipashwa kwamba katika uhakika ustawisho wa ushirika na uchumi wa kundi lote la wakaaji wa nafasi, lijiingize katika mpango wa ustawisho wa sehemu ya msitu ambamo wanapatikana. Katika ustawisho wa jimbo na hata pia ustawisho wa inchi nzima. Ijapokuwa ni uhakimu tu ndio unakuwa na yote ilio ya lazima kwa kuongoza mpango wa ustawisho wa inchi kwa namna yote ya kuyatumikisha.»[8]

Kwa hiyo, katika makubaliano, hawapashwe kusahau chumba cha Waziri anae husika na ustawisho wa miji na vijiji sababu Waziri huyo ana katika mamlaka yake pia: kutunga na kufatilia miradi za ustawisho wa vijiji, miji na pembeni ya miji mikuu; kutunga na kuongoza siasa ya ustawisho wa miji na vijiji, matengenezo na vyombo vya matumizi ya eneo la miji na vijiji; uongozi na kuingizwa kwa mipango ya ustawisho katika miji na vijiji; matengenezo, majengo, kurudishwa upia, matengenezo ya miundombinu ya ushirika na uchumi ni vya lazima katika eneo la vijiji na kandokando ya miji mikuu.

Kwa mwisho, kama inavyo andikwa na waandishi hawa wamoja, uhakimu ulipashwa kuwa na kazi ya muhimu katika makubaliano ya maneno inayo faa kwa kutimiza miundonmbinu ya ushirika na uchumi ya lazima. Kama vile wakati wa upekuzi wa watu wote, unao pashua kutimizwa, usio wakati tu wa kuwekwa kwa msitu wa mazao daima, lakini pia mbele ya kazi ya kupanwa kwa eneo la misitu.

Nani anapashwa kusimamia kundi ao vikundi vya wakaaji wa nafasi katika makubaliano ya maneno inayo angalia ushirika? Tunapashwa kujua kwamba shirika lote la wakaaji wa asili linalo ongozwa chini ya mila lina ongozwa na sultani aliye chaguliwa kwa njia ya mila, hata ikiwa kundi la wakaaji wa nafasi wanapatikana katika utawala wa chefferi ao sekta, amri ya 66 na 67 ya sheria ya ndani ya 7 Octoba 2008. Sheria moja hii inasema katika amri ya 85 na 86 kwamba kiongozi wa sekta na wa chefferie ni wajumbe wa milki yao mbele ya serikali na

[8]V. Vundu dia Massamba et G. Kalambay Lumpungu, Op.cit., p.65.

mbele ya watu wengine kwa hiyo wanapashwa patikana kati ya watu watakao fanya masikilizano na mpewaji wa msitu kwa maneno yanayo angalia ushirika.

Amri ya 88 inasema kwamba, mkataba wa eneo la msitu una sehemu mbili: mkataba mwenyewe. Unao hakikisha haki na sharti za sehemu zote. Na buku ya mahitaji yanayo onyesha sharti kawaida za mpewaji msitu; kwa ajili ya uhakikisho wa kuheshimishwa kwa sheria ya matumizi ya msitu. Heshima ya Mbinu na ya mambo yapatikanayo ndani ya buku ya mahitaji. Kwa siku 16/Juni 2009, ilikamatiwa sheria ya Waziri namba 102/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/09 kwa haya:

- Uhakiki unao heshimu sheria ya matumizi una angalia uchunguzi wa heshima ya mipango ya buku ya sheria ya msitu na ya namna ya kuyatumikisha. Na ina angalia zaidi heshima ya muda na uhakika wa vyeti vya matumizi, amri ya 4;
- Uhakiki wa kuheshimu mbinu, unangalia zaidi matumizi nzuri ya namna ya kuhesabu msitu, ya sheria ya mazingira, inayo ungwa na matumizi, pia kuheshimu wakati wa kushimikwa na kuanzishwa kwa mpango wa matengenezo kwa njia ya kanuni ya sasa, amri ya 5;
- Uhakiki unao husika na maneno yenye kupatikana ndani ya mkataba, unaangalia sawa vile juu: heshima ya yote yenye mpewaji wa msitu ao mtumikishaji wote wa pori, anaitika kutimiza kwa kusaidia ustawisho wa nafasi; kupitia miundombinu ya ushirika na uchumi na kuhakikisha maisha mazuri ya ushirika ya wafanya kazi wake, amri ya 6.

Kuto kuheshimu moja ya mambo, itampa serikali nguvu ya sheria ya kuvunja mkataba wa kupanwa kwa msitu. Na mpewaji wa msitu anasheria ya kuomba serkali arudilie makusudio yake mbele ya vyumba vya sheria vinavyo husika na mambo haya.

Imewezekana kukose masikilizano kati ya mpewaji wa msitu na kikundi ao vikundi vya wakaaji wa nafasi juu ya:

- Namna shirika za nafasi wanaweza kutimiza haki zao ndani ya msitu ulio pewa;
- Kutotimizwa ao kutimizwa kusio faa kwa fungo na yenye kupatikana ndani ya buku la mahitaji yenyi kuangalia matumizi ya miundombinu ya ushirika na uchumi;
- Kosa moja fulani lenye kutendewa wakaaji wanafasi kwa tendo la utumivu usiyo faa ya msitu iliyo panwa ao ujenzi mbovu wa msitu, amri ya 3.

Suluhisho ya mangonvi ina fanya msingi wa sheria ya Waziri namba 103/CAB/MIN/ECN-T/JEB/09 ya tarehe 16 Juni 2009 inayo angalia mipango juu ya magonvi ya misitu, kulishimikwa ndani ya kata yote kamati inayo husika na magonvi ya msitu.

Kamati hii inakutana ndani ya chumba cha kazi ya uhakimu wa kata unao husika na msitu.

Amri ya 9 mpaka 13 vinasema juu mwendeno mbele ya kamati. Kama moja ya vikundi haikufurahi na makusudi ya kamati, ina haki ya kupeleka mgogoro mbele ya chumba cha sheria ya juu kinacho julikana hivyo ndani ya kata.

Ndani ya mkataba wenyi kuunganisha vikundi vitatu, bila ubishi haikutosheka, vikundi vitatu hivyo vina haki na sharti, vimoja mbele ya vingine, vyenye vina stahili kuonyeshwa sasa.

## IV. HAKI NA SHARTI ZA SHIRIKA ZINAZO ELEKEWA

Wanao lazimishwa ndani ya mkataba wa kupanwa kwa eneo la msitu: serikali, mpewaji wa msitu, na kwa njia ya kusimamiwa, kikundi ao vikundi vya wakaaji wa nafasi.

**IV.1. Serikali Mwenyeji Manufaa**

| HAKI | SHARTI |
|---|---|
| **SHERIA YA MSITU (CODE FORESTIER DE 2002)** | |
| • Mwenyeji wa msitu, amri ya 7 na 10, sehemu ya 2 na 3;<br>• Kuweka masikilizano mkataba wa kupanwa kwa msitu, amri ya 88;<br>• Kuweza kuondoa ndani ya kata kwa kutumikisha miti ao eneo la muhimu kwa matumizi ya kazi ya faida kwa watu wote, amri ya 110; | • Mgao wa msitu, amri ya 42, sehemu ya 3;<br>• Kutunga siasa ya msitu ya taifa, amri ya 4 mpaka 6;<br>• Kuweka akiba pori zinazo kingwa kwa kufikia eneo 15% ya udongo wa taifa, amri ya 15;<br>• Kuwa na madaraka ya kuongoza, ku hakimu, ukingo, kuchunga na kijeshi ya ukingo wa msitu, amri ya 24;<br>• Kusaidia ustawisho wa kuvumbua msitu, amri ya 33 mpaka 35;<br>• Kujua hesabu ya msitu mbele ya matumizi ya |

<table>
<tr><td>

- Kukatazwa kwa mtumikishaji wa msitu, amri ya 114 mpaka 119;
- Kupangwa kwa bei ya kodi na malipo mbali mbali na namna ya kuyalipisha, amri ya 121 na 122;
- Kwazibu wasio itika kutimiza yanayo pangwa, amri ya 143 mpaka 154;
- Kutia mipango ya kutosha inje ya mipaka ya inchi mafuta fulani, amri ya 94;
- Kuruhusu mpangisho kulipiza, kupana, kubadilisha ao kupanwa kwa eneo ya msitu, amri ya 95.

</td><td>

misitu yote, amri ya 65;

- Kujua kwa wakati wote hesabu ya msitu wa inchi, amri ya 66;
- Kugawanya eneo la msitu kwa sehemu ya msitu ya ujenzi, amri ya 71 mpaka 75;
- Kutangulisha kazi zote za matumizi na matumikisho ya msitu na mpango wa ujenzi wa msitu, amri ya 76;
- Kuhakikisha kurudishwa upia manufaa ya msitu, amri ya 77 na 78;
- Kugaramia kwa vikundi vyote sehemu yao ya mali inayo toka kwa kodi na malipo mbalimbali, amri ya 122;
- Kufanya ujuvi wa watu wote kwa kujua maumbile na uwezo wa haki za watu wengine juu ya msitu ya kupanwa, amri ya 84;
- Kuuzisha kwa watu wote pori za kupanwa, amri ya 83 na 85;
- Kuomba mpewaji wa msitu kuheshimu maneno ya upekee yanao patikana ndani ya buku la mahitaji kwa faida ya vikundi vya wakaaji wa nafasi, amri ya 89.

</td></tr>
<tr><td colspan="2">SHERIA N°08/09 YA 08 APRILI 2008 INAYO PANGA NAMNA YA KUPANA SEHEMU YA ENEO LA MSITU</td></tr>
<tr><td></td><td>

- Kufanya buku la mahitaji ya muuzishaji kwa watu wote kupitia uhakimu, amri ya 40;
- Kufanya ujuvi wa mupatano na wakaaji wa nafasi kwa kuandika buku la mahitaji kwa kuuzishwa kwa watu wote, amri ya 40.

</td></tr>
<tr><td colspan="2">SHERIA YA WAZIRI N° 028/CAB/MIN/ECN –T/15/JEB/08 YA TEREHE 7 AGOSTI 2008 INAYO PANGA NAMNA YA MIKATABA YA ENEO YA MSITU YA KUTUMIKISHWA KWA KUKATA MITI NA YA BUKU LA MAHITAJI<br>KIBAMBO CHA I</td></tr>
<tr><td>

- Wakati mpango mmoja wa mkataba na wa buku la mahitaji hau kuheshimiwa, ya faa kukataa kurudisha pia mkataba wa eneo la msitu, amri ya 8;

</td><td>

- Kugaramia kwa mmiliki wa misitu uwezo wote wa kutumia haki anazo pewa na buku la sheria ya msitu, amri ya 4.

</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| • Kwa yote yanayo patikanamo katika amri ya 23 inaleta uwezo wa kuvunja mkataba wa eneo la msitu, amri ya 24. | |

**IV.2. Miliki Wa Msitu**

| HAKI | SHARTI |
|---|---|
| **KITABU CHA SHERIA LA MSITU (CODE FORESTIER DE 2002)** | |
| • Kutia saini mkataba wa eneo la msitu, amri ya 92;<br>• Kutumikisha sehemu iliyo panwa, amri ya 90;<br>• Kutia kitambulisho cha miti yote inayoweza kutumikishwa, amri ya 94;<br>• Kufungua njia ya watu wote ya kubebea mazao, amri ya 103;<br>• Kutumia kwa upekee njia ya kubeba mazao iliyo tengenezwa na amri ya 106;<br>• Kulipwa haki ikiwa serikali anarudilia eneo lake, amri ya 110. | • Kutunga na kutumikisha mpango wa matumikisho ya eneo la msitu, amri ya 76 na 99;<br>• Kupana pesa ya akiba kwa benki fulani, amri ya 82;<br>• Kulipa kodi na yote yanayo faa kwa kutumikisha msitu, amri ya 93 na 121;<br>• Mbele ya matumikisho yote kufanya hesabu ya misitu, amri ya 100;<br>• Kuacha huru kwa uhakimu na kwa wana memba wa kamati ya jimbo inayo angalia majuviano, na kutembelea eneo la msitu, amri ya 105;<br>• Kuheshimu mipamgo ya uhakika na ya kupanga mazao ya msitu isiyo geuzwa, amri ya 108;<br>• Kutumia nyundo (ao saini ya mutumizi) ya msitu, amri ya 108;<br>• Kuheshimu muda wa kutumikisha, amri ya 114;<br>• Kujenga makao na kutumikisha msitu katika muda ulio kubalika, amri ya 115. |
| **SHERIA N°08/09 YA TEREHE 08 APRILI 2008 INAYO PANGA NAMNA YA KUGAWA ENEO LA MSITU** | |
| • Kwa mwenyeji wa faida zinazo toka katika hala la hifadhi, amri ya 40. | • Kupeleka pesa ya akiba katika muda wa siku 30, amri ya 34. |
| **SHERIA YA WAZIRI N0 028/CAB/MIN/ECN –T/15/JEB/08 YA TAREHE 7 AGOSTI 2008 INAYO PANGA NAMNA YA MKATABA WA ENEO LA MSITU, GINSI YA MATIMIZI YA MAZAO YA MSITU NA YA KITABU CHA MAHITAJI**<br>**KIBAMBO CHA I** | |
| • Kutumikisha kwa namna ya upekee miti ya kuchora katika eneo | • Kuheshimu haki ya matumizi ya kale ya vikundi vya wakaaji wa nafasi, amri ya 6; |

| | |
|---|---|
| la msitu, amri ya 5;<br>• Kupewa ruhusa kwa kuweka njia ya kupitia kwa mwisho wa eneo la kandokando, amri ya 7;<br>• Kuomba kurudishwa upia mkataba wa eneo ya pori, amri ya 8;<br>• Kukubali bila shaka kuondosha faida ya eneo la msitu mbele ya kumalizika kwa mkataba wa eneo la msitu, amri ya 22. | • Kuweka kikao katika sehemu iliyo panwa na kupatumikisha haki na sharti zao, amri ya 9;<br>• Kutayarisha na kuyatoa kwa makubaliano, mipango na matengenezo, amri ya 10;<br>• Kuheshimu sheria mpango inayo angalia mazingira na kuchunga maisha mbalimbali, amri ya 11;<br>• Kuheshimu kuchunga ao kuweka pembeni kwa kuchunga namna mbalimbali ya mazao mapya, amri ya 12;<br>• Kutia mipaka ya eneo la pori lako kwa alama zinazo onekana, amri ya 13;<br>• Kutia rangi ao alama miti zilizo katwa, amri ya 16;<br>• Kutimiza majengo inayodumu ya shirika, uchumi na ya kazi ya shirika kwa faida ya vikundi vya wakaaji wa nafasi kama inavyo hitajika katika kitabu cha mahitaji, amri ya 17;<br>• Kujuviana (kupatana) na wakaaji wa nafasi kwa ajili ya miundombinu ya ushirika, uchumi na ya kazi ya shirika, amri ya 17;<br>• Kulipa bila kupitisha muda na kwa wakati, kodi na yote yanayo ombwa kwa ajili ya msitu, amri ya 19;<br>• Kuweka polisi wa usalama, amri ya 20. |
| **SHERIA YA WAZIRI N0 028/CAB/MIN/ECN –T/15/JEB/08 YA TAREHE 7 AGOSTI 2008 INAYOTOA MPANGO JUU YA MKATABA WA ENEO LA MSITU YA MATUMZI YA MAZAO YA MSITU NA YA KITABU CHA MAHITAJI**<br>**KIBAMBO CHA II** | |
| | • Kutengeneza katika muda wote wa kutumikisha mkataba wa eneo mipaka ambazo zinapashwa kusafishwa kusudi ya kuonekana waziwazi, amri ya 2;<br>• Kuandikia viongozi ao serikali ya nafasi kwa ajili ya mpango wa matumizi na kuyajulisha vikundi vya wakaaji wa nafasi, amri ya 3;<br>• Kupewa na uhakimu ruhusa kwa mwaka mzima juu ya kukata miti, amri ya 4;<br>• Kuchunga katika ofisi ilio katika kata ya eneo la msitu, vibaruwa yote ya lazima kwa matumikisho, kuchunga na kuchungua kazi za matumikisho |

| | |
|---|---|
| | yote ya eneo la msitu, amri ya 6;<br>• Kuchunga katika kiwanda buku lote linalo onesha hesabu ao matokeo inayo angalia majengo kugeuzwa na kuuzishwa kwa miti, amri ya 6;<br>• Hapana kuleta magumu kwa wakaaji wa nafasi wa kandokando ya eneo la msitu, kutumikisha haki zao za asili juu ya msitu, amri ya 7;<br>• Kusaidia uchaguzi na ufundi wa matumizi kutoka vikundi vya wakaaji wa nafasi, amri ya 8;<br>• Kuleta kwa watumishi vyombo vya kazi vya usafi na ukingo vinavyo faa kwa fasi zote za kazi, amri ya 9;<br>• Kupokea na kushimika vyombo vya kutumikisha na vya kugeuza kama inavyo ombwa katika matumizi yao, amri ya 10;<br>• Kupanga na kutumikisha mpango wa kuleta heshima ya miti zilizo katwa kutoka eneo la msitu, amri ya 11. |

**IV.3. Wakaaji Na Shirika La Nafasi**

| HAKI | SHARTI |
|---|---|
| • Kuomba sehemu ao msitu mzima kwa namna ya eneo la msitu ya kutumikisha, amri ya 22, sheria ya misitu (Code forestier, C.F.);<br>• Kutumikisha msitu ulio pewa, amri ya 112 C.F.;<br>• Mwenyeji miti inayo patikana katika muji na kandokando yake, amri ya 9 C.F.;<br>• Kuulizwa mbele ya kupangwa kwa msitu, amri ya 15 C.F.;<br>• Kushiriki kwa ujuvi wote wa watu uchunguzi wa umma unao tangulia mkataba wa eneo la msitu wa kupanwa, amri ya 84 C.F.;<br>• Kuacha huru wakaaji wa kandokando kutumikisha haki hizi katika msitu unao pangwa, amri ya 38 na 39 CF:<br>- Kuokota kuni na magungu na nyasi;<br>- Kuchuma matunda, miti inayotoa mazao ya kula ao ya uganga;<br>- Kuvuna matunda (utonvi), matunda | • Kuheshimu haki ya matumizi kama inavyo ombwa katika kila namna ya msitu, amri ya 36 C.F.;<br>• Kutofanya ukulima ao namna zote za kazi zinazo weza leta magumu kwa matengenezo yanayo dumu za msitu ya kupangwa na kwa matumizi ya eneo la msitu, amri ya 39 na ya 44 C.F.;<br>• Kuhakikisha kwa mtumiaji wa msitu ukimya katika matumizi ya eneo lake la msitu;<br>• Kuheshimu haki zinazo patikana kutoka kitabu cha mahitaji. |

| | |
|---|---|
| ya RESINES na asali;<br>- Kuokota vidudu vya kula, kola ao vyura;<br>- Uchaguzi wa miti ya majengo ya nyumba ya asili, makao ao vijiji.<br>• Kufanyika tu na wakaaji wa kandokando haki ya asili ya matumizi katika msitu wa mazao yanayo dumu, isiyo na shida kwa matumikisho ya msitu kuondoa ukulima, amri ya 44 C.F.;<br>• Kuomba makubaliano ya ushirika ya kitabu cha mahitaji ya mkataba wa eneo la msitu wa kupanwa kwa mambo yanayo angalia majengo ya kudumu ya ushirika na uchumi, amri ya 17 cha sheria ya Waziri 028, kibambo cha 1 na amri ya 13, cha sheria ya Waziri 028 kibambo cha 2;<br>• Kuomba msaada wa watu wengine kwa kutumikisha eneo la msitu ulio pewa: uhakimu ao mtumizi wa asili, amri ya 112 na 113 C.F. | |

# V. KWA KUMALIZA

Ikiwa serikali katika mkataba wa eneo la msitu ya kupewa ndiye mmoja wa wenye kufanya mkataba na alie na faida kubwa, kupitia taswira hizi zilizo juu, mtumishi ao mmiliki wa msitu yeye ana sharti nyingi hizi zilizo mizigo juu bahati yake, zina kombolewa na faida anayo itoa katika kutumikisha msitu. Inasemwa katika kitabu cha haki «hakuna kazi bila faida».

Kutumikisha msitu kunaleta faida ya uchumi kwa serikali kupitia kodi na mapashwa mbalimbali ambazo mpewaji wa msitu anapashwa kuleta na kundi ao vikundi vya wakaaji wa nafasi kupitia utimivu ao kushimikwa kwa majengo yanayo dumu ya ushirika na uchumi na ya kazi za shirika.

Kwa ginsi miundombinu ya ushirika na uchumi itwoe matunda ao manufaa yanayo onekana, ya faa kuyaongeza pamoja na ya kata, ya wilaya na jimbo. Ni kwa ajili hiyo ina ombwa makubaliano kati ya uhakimu na vikundi vya kazi visivyo vya serikali, vinavyo saidia vikundi vya wakaaji wa nafasi kwa kutengeneza maisha yao vizuri.

# VI. VITABU VILIVYO TUMIWA

**VI.1. Niaraka halali**


- Loi n°71-008 du 31 décembre 1971 portant révision de la Constitution de 1967.
- Loi 73-021 du 20 juillet 1973 portant régime général des biens, régime foncier et immobilier et régime des sûretés, Journal officiel, 1974, 1er février 1974, p.69.
- Décret-loi 081 du 2 juillet 1998 portant organisation territoriale et administrative de la République Démocratique du Congo, Codes Larcier, T.III, Vol.1, p.23.
- Constitution de la République Démocratique du Congo du 18 février 2006.
- Loi n°08-012 du 31 juillet 2008 portant principes fondamentaux relatifs à la libre administration des provinces, Journal officiel du 31 juillet 2008.
- Arrêté ministériel n°024/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/08 du 7 août 2008 fixant la procédure d'enquête publique préalable à l'octroi des concessions forestières, Journal officiel du 30 septembre 2008, col.48.
- Arrêté ministériel n°028/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/08 du 7 août 2008 fixant les modèles de contrat de concession d'exploitation des produits forestiers et de cahiers des charges y afférents, Journal officiel du 30 septembre 2008, col.66.

- Loi organique n°08-016 du 7 octobre portant composition, organisation et fonctionnement des entités territoriales décentralisées et leurs rapports avec l'Etat et les provinces, Journal officiel du 10 octobre.
- Arrêté ministériel n° 102/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/09 du 16 juin 2009 fixant les règles et les formalités du contrôle forestier, Journal officiel du 1er juillet 2009, col.25.
- Arrêté ministériel n°103/CAB/MIN/ECN-T/15/JEB/09 du 16 juin 2009 portant organisation et fonctionnement de la commission de règlement des différends forestiers, Journal officiel du 1er juillet 2009, col.34.

**VI.2. Vitabu Ao Maandiko Mbalimbali**

De SADELEER (N)

Vade-Mecum sur le droit international de la biodiversité, Bruxelles, Cèdre, 2003, 338p.

Ministère de l'Environnement, Conservation de la Nature et Tourisme

Guide pratique pour les négociations entre les concessionnaires forestiers et les communautés locales et / ou peuples autochtones sur la clause sociale du cahier des charges, Kinshasa, Mai 2010, 29p.

VUNDU dia MASSAMBA (V) et KALAMBAY LUMPUNGU (G)

Le code forestier commenté et annoté. Loi n°11-2002 du 29 août 2002, Kinshasa, 109p.

**Traduction réalisée par l'ONGD "EDEN"**